Somo la 13　小説が好きです
SHÔSETSU GA SUKI DESU

さくら	ロドリゴさんの趣味は何ですか。	Rodrigo, unapenda nini?
Sakura	RODORIGO-SAN NO SHUMI WA NAN DESU KA.	
ロドリゴ	読書です。特に歴史小説が好きです。	Kusoma vitabu.
Rodrigo	DOKUSHO DESU. TOKUNI REKISHI SHÔSETSU GA SUKI DESU.	Ninachopenda hasa ni riwaya za historia.
さくら	へえ。新宿に新しい本屋が出来ましたよ。	Aha! Kuna duka jipya la vitabu limefunguliwa Shinjuku.
Sakura	みんなで行きませんか。	Kwa nini tusiende pamoja?
	HÊ. SHINJUKU NI ATARASHII HON-YA GA DEKIMASHITA YO. MINNA DE IKIMASEN KA.	

Vidokezo vya sarufi

① **Nomino-A WA Nomino-B GA SUKI DESU**　(A anapenda B)

◈ SUKI ni kivumishi kinachomaanisha “kupenda.”

◈ Kwa muktadha huu, GA inaonyesha lengo la kivumishi.

k.m.) ANNA WA MANGA GA SUKI DESU. (Anna anapenda MANGA.)

② **_ MASEN KA**　(Kwa nini tusifanye _?)

◈ Ikiwa utabadilisha MASU kwenda kwenye MASEN KA, unawaalika watu wafanye jambo fulani.

k.m.) MINNA DE HON-YA NI IKIMASU.　(Tutaenda kwenye duka la vitabu pamoja.)

⇒ MINNA DE HON-YA NI IKIMASEN KA. (Unaonaje tukienda pamoja kwenye duka la vitabu?)

③ **Aina 2 za vivumishi**　☞ *Vivumishi : uk.53*

◈ Vivumishi vimegawanyika katika aina mbili.

Vile vinavyomalizikia na silabi I vinaitwa vivumishi vya I. Vingine vinaitwa vivumishi vya NA.

Vivumishi vya I　:　ATARASHII (mpya)　ATARASHII HON (kitabu kipya)

Vivumishi vya NA　:　SUKI (kupenda)　SUKINA HON (kitabu ninachopenda)

Tanakali Sauti

KIRAKIRA

Inaelezea vile ambavyo kitu kinang’aa au kumeremeta.

PIKAPIKA

Inaelezea jinsi kitu kinavyong’aa baada ya kusafishwa.

Imetayarishwa na NHK WORLD © ver. April 2015